CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO CHUO KIKUU CHA DODOMA

(UDOM SACCOS LTD)

NAMBARI YA USAJILI:

PRI-DOM-DOM-CC-2022-130

SERA YA UUZAJI WA MALI ZA CHAMA

Imeandaliwa na:
S.L.P 2765, DODOMA
Email:udomsaccosltd@gmail.com
Bodi ya UDOM SACCOS LTD

TOLEO LA 1 , 2025

YALIYOMO

DIBAJI 2

TAFSIRI YA MANENO 3

SEHEMU YA KWANZA 6

UTANGULIZI 6

1.2 Chimbuko la Sera 6

SEHEMU YA PILI 7

MALENGO, WALENGWA WA SERA HII PAMOJA NA TARATIBU ZA UUZAJI MALI 7

2.1 Lengo na Madhumuni ya Sera 7

2.3 Taratibu zinazopaswa kuzingatiwa na Chama kabla ya kuuza mali 7

2.4 Hatua za kufuata wakati wa kuuza mali za Chama; 8

2.4.1 Utambuzi wa Mali iliyokusudiwa kuuzwa 8

2.4.2 Utambuzi wa Mali iliyokusudiwa kuuzwa 8

2.4.3 Utambuzi wa Mali iliyokusudiwa kuuzwa 8

2.4.4 Utambuzi wa Mali iliyokusudiwa kuuzwa 8

2.4.5 Uuzaji wa Mali 9

2.4.2 Kuondoa Mali katika Vitabu vya Chama 9

Baada ya mali kuuzwa, Chama kitatakiwa kufuta mali hiyo katika vitabu vyake na kuondoa nyaraka zote zinazohusiana na mali hiyo. 9

SEHEMU YA TATU 10

MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA UTOAJI WA VIBALI VYA UUZAJI WA MALI ZA CHAMA 10

SEHEMU YA NNE 11

4.0 UFAFANUZI WA JUMLA 11

4.1 Taratibu za Utoaji Vibali 11

4.2 Maswali yanayopaswa kuzingatiwa kabla ya kutoa kibali 11

SEHEMU YA TANO 13

HITIMISHO 13

DIBAJI

Umiliki wa mali katika vyama vya ushirika nchini umekuwa kila siku kutokana na mamlaka yanayotolewa na kifungu cha 35 cha sharia ya vyama vya ushirika Na. 06 ya mwaka 2013. Aidha, pamoja na vyama hivyo kuwa na haki ya kumiliki mali, wakati mwingine katika uendeshaji na utoaji wa huduma kwa wanachama, Vyama hutaka kuuza mali vinazomiliki kutokana na uchakavu wa mali ulipaji wa madeni au kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Kutokana na changamoto zinazojitokeza wakati wa uuzaji wa mali za vyama ushirika nchini,Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika iliandaa mwongozo ambao umekuwa ni chanzo cha upatikanaji wa sera hii ukiainisha utarativu utakaotumika katika uuzaji wa mali za Chama.

Sera hii imelenga kufafanua taratibu za msingi za kufuatwa katika uuzaji wa mali za Chama. Taratibu hizo zinatakiwa kuzingatiwa na chama wakati wa hitaji la kuuza mali ili kupunguza migogoro inayoweza kujitokeza mara baada ya kuuzwa kwa mali hizo.

TAFSIRI YA MANENO

Kuanza kutumika kwa sera hii

1 Sera hii itajulikana kama sera ya Uuzaji wa Mali za Chama na itaanza kutumika mara baada ya kupitishwa na kuidhinishwa na kusajiliwa na Mrajis.

Tafsiri

2 Katika sera hii, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo maneno yaliyoainishwa hapa chini yatakuwa na maana iliyotolewa:

a) **"Afisa"** maana yake ni mtu mwenye wadhifa wa kuchaguliwa au kuajiriwa katika Chama ambaye atajumuisha Meneja Mkuu, Mhasibu Mkuu, Mkaguzi wa Ndani, Mhazini na wengine waliopewa mamlaka chini ya sera hii ya chama;

b) **"Mjumbe wa Bodi"** maana yake ni mtu mwenye wadhifa wa kuchaguliwa au kuajiriwa katika Chama ambaye atajumuisha Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wa Bodi, Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi.

c) **"Meneja"** ni mtendaji mkuu wa Chama anayesimamia utendaji wa ujumla wa sera, matukio ya Chama na Bajeti na ni msemaji wa Chama kwa upande wa Menejimenti.

d) **"Afisa Mikopo"** itakuwa na maana ya mtu aliyeajiriwa na Chama kwa ajili ya kupitia na kuchambua maombi ya mikopo yanayowasilishwa na wanachama na kufanya ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo hiyo;

e) **"Sheria"** ni mfumo wa kanuni ambazo hutekelezwa na taasisi maalumukatika Nyanja ya siasa, uchumi, na jamii kwa njia mbalimbali na huratibu mahusiano baina ya watu. Mifumo ya sheria inaeleza haki na wajibu wa kila mmoja.

f) **"Mrajis Msaidizi"** ni kiongozi wa vyama vya ushirika Mkoa anayeteuliwa na Mrajis wa taifa wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa ajili ya kuongoza ushirika katika Mkoa;

g) **"Bodi ya Uongozi"** maana yake ni chombo kilichochaguliwa na wanachama kupitia Mkutano Mkuu kwa ajili ya kusimamia shughuli za kila siku za chama;

h) **"Chama"** maana yake ni Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo Chuo kikuu cha Dodoma (UDOM SACCOS LTD) kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika;

i) **"Dhamana"** ni kitu chochote ambacho mtu anaweka au kuwekewa ili kukomboa kitu fulani au kupata huduma fulani. Dhamana inaweza kuwa fedha, gari, nyumba na hata chochote kile;

j) **"Mkataba"** ni makubaliano ya kisheria kati ya watu wawili au zaidi au wahusika ambapo katika sera hii ni baina ya mkopeshaji au mkusanya madeni na mkopaji.

k) **"Mdhamini"** maana yake ni mwanachama anayemchukulia mwanachama mwingine dhamana kuwa atatimiza jambo fulani;

l) **"Adhabu"** maana yake ni fedha analolipa mwanachama kwa kutorejesha marejesho ya mkopo kwa muda uliopangwa;

m) **"Mrajis"** maana yake ni kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013;

n) **"Sera/Mwongozo"** maana yake ni utaratibu uliowekwa na wanachama kuongoza watendaji wa Chama katika uendeshaji wa shughuli za chama ili kufikia malengo yaliyowekwa kwa manufaa ya wanachama;

o) **"Sheria"** ina maana ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 pamoja na Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na. 10 ya Mwaka 2018;

p) **"Tume"** ina maana Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC);

q) **"Mali"** ni chochote kinachoweza kumilikiwa na Chama kinaweza kuhamishika au kisichoweza kuhamishika;

r) "Kibali" ni idhini inayotolewa na Mamlaka husika kwa ajili ya kuzingatia utaratibu wa kiutendaji.

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Historia ya Ushirika nchini inaanzia kabla ya uhuru wa Tanganyika ambapo jamii ilielimishwa kuhusu umuhimu na manufaa ya kuwa na Vyama vya Ushirika, ili waweze kujikwamua kiuchumi na kijamii. Jamii ilihamasika na ikapelekea kuanzishwa kwa Vyama vya ushirika vya aina mbalimbali, kutegemeana na shughuli za kiuchumi na kijamii zinaendeshwa na Vyama hivyo, pamoja na mahitaji ya jamii husika.

Vyama vya Ushirika vimekuwa vikimiliki mali mbalimbali kama vile; Ardhi, Majengo, Magari na Mitambo, Samani, Hisa pamoja na mali nyinginezo kwa mujibu wa kifungu cha 35 sheria ya vyama vya ushirika Na. 06 ya mwaka 2013.

Pamoja na Vyama vya Ushirika kuwa na uwezo wa kumiliki mali, vyama hivi pia vinao uwezo wa kuuza mali vinazozimiliki kwa mujibu wa sharia ya Vyama vya ushirika ya mwaka 2015. Hivyo, Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM SACCOS LTD) kimeandaaa sera hiii kwa ajili ya kutoa utaratibu utakaotumika katika uuzaji wa mali za Chama.

1.2 Chimbuko la Sera

Sera hii imetokana na kutokuwepo kwa utaratibu ulioainishwa kwenye sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika, kuhusiana na taratibu zinazopaswa kuzingatiwa na Chama kuhusiana na uuzaji wa mali za chama nchini. Aidha,kutokana na kutokuwepo kwa uaratibu huo kumesababisha uwepo wa changamoto na malalamiko kuhsiana na namna ambavyo baadhi ya Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Ushirika wanacyouza mali za Chama pasipo kuzingatia bei halisi ya soko, thamani ya mali husika pmoja na hitaji la Chama husika kimiliki mali hizo.

SEHEMU YA PILI

MALENGO, WALENGWA WA SERA HII PAMOJA NA TARATIBU ZA UUZAJI MALI

2.1 Malengo ya Sera hii

2.1 Lengo na Madhumuni ya Sera

2.1.1 Lengo kuu

Lengo la Sera hii ni kuweka utaratibu wa uuzaji wa mali katika chama cha ushirika cha UDOM SACCOS LTD kwa ufanisi kwa kuzingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na taratibu za uendeshaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika na Sheria nyingine za Nchi.

2.2 Walengwa wa Sera hii

Sera hii umeandaliwa kwa ajili ya kutumiwa na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

(i) Maafisa Ushirika;
(ii) Wanachama, Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Ushirika;
(iii) Watendaji na viongozi wa Wizara za Kisekta, Mamlaka za Serikali, na taasisi mbalimbali za umma zinazofanya kazi na Vyama vya Ushirika; na
(iv) Wadau wengine wa maendeleo.

2.3 Taratibu zinazopaswa kuzingatiwa na Chama kabla ya kuuza mali

Wakatii wa uuzaji wa mali zake chama kinapaswa kuzingatia ifuatavyo:

(i) Uwepo wa sababu zinathibitisha umuhimu wa kuuzwa kwa mali husika;
(ii) Uwepo wa Azimio la Mkutano Mkuu ulioridhia kuuzwa kwa mali husika;
(iii) Uwepo wa nyaraka halisi (original document) za umiliki wa mali inayotakiwa kuuzwa na chama;

(iv) Uwepo wa taarifa ya uthaminishaji wa mali uliofanywa na mtaalamu anaetambulika kisheria; na
(v) Uwepo wa Mpango wa matumizi ya fedha.

2.4 Hatua za kufuata wakati wa kuuza mali za Chama;

2.4.1 Utambuzi wa Mali iliyokusudiwa kuuzwa

Chama cha ushirika kinachokusudia kuuza mali zake kitatakiwa kufanya yafuatayo: -

(i) Kuanisha mali inayotarajiwa kuuzwa;
(ii) Kuandaa nyaraka zote za umiliki wa mali hiyo; na
(iii) Kujiridhisha katika mamlaka husika juu ya umiliki wa mali hiyo.

2.4.2 Utambuzi wa Mali iliyokusudiwa kuuzwa

Baada ya kuridhika na sababu za kuuza mali, Bodi ya Chama itawasilisha katika Mkutano Mkuu nia yao ya kuuza mali ili kupata idhini sawa na matakwa ya kanuni ya 76(1) ya kanuni za vyama vya ushirika ya mwaka 2015

2.4.3 Utambuzi wa Mali iliyokusudiwa kuuzwa

Baada ya kupata idhini ya kuuza mali husika katika Mkutao Mkuu, Bodi ya Chama inapaswa kuthaminisha mali husika ili kupata thamani halisi kabla ya kuuza. Uthaminishaji wa mali ya Chama cha Ushirika utafanywa na mthamini anayetambulika na sheria ya uthaminishaji.

2.4.4 Utambuzi wa Mali iliyokusudiwa kuuzwa

Baada ya kukamilisha taratibu za uthaminishaji na kupata idhini ya Mkutano Mkuu, UDOM SACCOS LTD itaomba kibali cha kuuza mali husika kwa Mrajis wa Vyama vya ushirika. Kwa mali isiyozidi thamani ya shilingi bilioni moja (Tshs 1,000,000,000/=) kibali kitatolewa na waziri mwenye dhamana ya maendeleo ya ushirika.
Aidha, maombi yote ya kibali cha kuuza mali ya Chama cha Ushirika yenye thamani inayozidi shilingi bilioni moja (Tshs 1,000,000,000/=) yatapitishwa

kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika kabla ya kuwasilishwa kwa waziri mwenye dhamana ya maendeleo ya ushirika.

2.4.5 Uuzaji wa Mali

Baada ya kukamilika hatua zote zilizotajwa hapo juu, Chama kitauza Mali husika kwa njia itakayokuwa imeainishwa kwenye kibali cha kuuza mali hiyo.

2.4.2 Kuondoa Mali katika Vitabu vya Chama

Baada ya mali kuuzwa, Chama kitatakiwa kufuta mali hiyo katika vitabu vyake na kuondoa nyaraka zote zinazohusiana na mali hiyo.

SEHEMU YA TATU

MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA UTOAJI WA VIBALI VYA UUZAJI WA MALI ZA CHAMA

Wakati wa ushughulikiaji wa maombi ya vibali vya kuuza mali za Chama, Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika itapaswa kuzingatia mambo yafuatayo, kabla na wakati wa utoaji wa vibali husika: -

(i) Uhalali wa umiliki wa mali inayoombewa kibali cha kuuzwa (vyeti au hati na mizania ya Chama);

(ii) Uwepo wa ridhaa ya wanachama wa UDOM SACCOS LTD na Bodi ya Uongozi kinachoomba kibali (Muhtasasri wa kikao cha Bodi na Mkutano Mkuu, wenye Agenda ya uuzaji wa Mali);

(iii) Taarifa ya uthaminishaji wa Mali inayoombewa kuuzwa (taarifa iwe ya uthamini uliofanyika ndani ya kipindi cha miezi 6 wakati kibali kinaombwa)

(iv) Uthibitisho kutoka katika Chama kuwa Mali inayoombewa kibali haina mgogoro wowote au kuwekwa dhamana kwa ajili ya Mkopo; na

(v) Nyaraka nyingine yoyote ambayo Mrajis ataona inafaa, ili kujiridhisha.

SEHEMU YA NNE

4.0 UFAFANUZI WA JUMLA

4.1 Taratibu za Utoaji Vibali

Utaratibu wa utoaji wa Vibali vya Uuzaji Mali, utagawanywa katika makundi mawili ambayo ni: -

(i) Mali zitakazotolewa kibali na Mrajis wa Vyama vya Ushirika; na

(ii) Mali zitakazo tolewa kibali na Waziri mwenye dhamana ya Ushrika

Ufafanuzi wa utaratibu wa Uuza ji mali ni kama ifuatavyo:-

(i) Kwa mali zote zenye thamani ya Tshs 1,000,000,000/=, vibali vyake vitatolewa naMrajis wa Vyama vya Ushirika; na

(ii) Mali zote zenye thamani ya Tshs 1,000,000,000/= vibali vyake vitatolwa na Waziri mwenye dhamana ya maendeleo ya Ushirika, baada ya kuwasilishwa kwake na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

4.2 Maswali yanayopaswa kuzingatiwa kabla ya kutoa kibali

Utaratibu wa uuzaji wa mali za UDOM SACCOS LTD utazingatia mambo yafatayo: -

(i) Maombi yote ya vibali vya uuzaji wa mali, yanapaswa kuwasilishwa kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika, yakiwa na

a) barua ya maombi;
b) Taarifa za uthaminishaji wa mali;
c) Mihutasari ya Vikao Vya Bodi na Nikutano Mikuu; na
d) Pamoja na taarifa nyingine ambazo zitaonekana kuasaidia upatikanaji wa vibali husika.

(ii) Njia ya uuzwaji wa Mali hizo au hiyo zitaanishwa katika kibali kitakachotolewa;

(iii) Mali iliyopewa kibali cha kuuzwa, itauzwa kwa thamani isiyopungua ile iliyoainishwa kwenye taarifa ya uthaminishaji wa mali husika. Endapo thamani hiyo haitafikiwa, ni lazima kuombwa kibali kwa aliyekitoa kuuza mali husika;

(iv) Kibali kitakachotolewa kitakuwa cha muda wa mwaka mmoja pekee, na iwapo muda huo utaisha pasipo kuuzwa mali husika, kibali husika kitapaswa kuombwa upya; na

(v) Sera hii itahusisha, Mali za UDOM SACCOS LTD zinazoombewa kuuzwa wakati Chama kinafanya kazi.

(vi) Endapo UDOM SACCOS LTD itafutwa, Wafilisi wataendelea na uuzaji wa Mali zake na kulipa madeni kama ilivyoelekezwa katika mwongozo wa ufilisi wa mwaka 2022 uliotolewa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

SEHEMU YA TANO

HITIMISHO

UDOM SACCOS LTD pamoja na Wadau wake wanaotaka kununua mali za Chama wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa katika sera hii na hatimaye kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa ili kuwa na chama imara vinavyozingatia sharia, kanuni na taratibu za kiushririka kwa maslahi mapana ya Chama, wanachama na Taifa kwa ujumla.

Aidha, sera hii itasomwa pamoja na sera ya manunuzi Chama na ikiwa sera hii itahitahi ufafanuzi wadau wanaohusika watatakiwa kuwasiliana na Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

Sera hii itafanyiwa maboresho (marekebisho) mara kwa mara ili kurekebisha, kuongeza jambo pale itakapoonekana kuwa inalazimu kufanya hivyo kwa maslahi ya wanachama kadiri ya Bodi na Mkutano Mkuu itakavyoonesha inafaa. Maboresho yoyote yatafanyika kwa kuzingatia sharia ya Vyama vya ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 na kanuni za SACCOS 2014.

Sera hii imetayarishwa na Bodi ya UDOM SACCOS LTD na baadae ya kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Bodi wa Chama uliofanyika tarehe 14/10/2025.

_____

Mrajis Msaidizi (M) Dodoma

Tarehe_____